MAFUNZO YA UFIKIKAJI NA UJUMUISHI 2021

Abilis Foundation sr

actalliance TANZANIA FORUM

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA

Embassy of Finland Dar es Salaam

Felm 1859

fida

MKUKI UKATIKI

sense international

UNFPA

WiLDAF TANZANIA

MKUKI
MAFUNZO YA UFIKIKAJI NA UJUMUISHI

25 Oktoba 2021

Katika Maandalizi ya Siku 16 za Uanaharakati

Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

With support from
Finland's development
cooperation

(Picha ya mbele imetolewa na Abilis Foundation)

Mandharinyuma

Tangu mwaka 1991, kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia (UWAKI) umemulikia taa suala la ukatili dhidi ya wanawake na wasichana. Hata hivyo, aghalabu sauti za watu wenye vilema hazisikiki kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu ya kuwezesha ufikikaji. Kwenye mchakato kuelekea kampeni ya Siku 16 ya mwaka 2021 Tanzania, Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) wametoa mafunzo ya ufikikaji kwa ajili ya wadau katika nafasi ya UWAKI, kwa hisani ya mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu yakiwemo mashirika ya Kifini ya Abilis Foundation, Fida International, Felm, wakichangiwa na Sense International Pamoja na UNFPA. Madhumuni ya mafunzo haya yalikuwa ni kuziba mianya ya ujuzi na kuwapa wadau zana za kuhakikisha ufikikaji katika nafasi halisi na pepe.

Kuzingatia janga la UVIKO-19, mafunzo haya yalifanya mtandaoni kwenye jukwaa la Zoom. Ushiriki ulitambuliwa kuwa mzuri kuliko mafunzo mengine ya awali ya MKUKI na mahudhurio yalionyesha uwakilishi kutoka sekta mbalimbali ikiwemo serikali na mashirika yasio ya kiserikali kutoka pande kadhaa za nchi. Wanawake kwenye vilema waliwakilishwa vema, na pia wakalimani wa Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) walikuwepo. Mafunzo yalikuwa shirikishi mno na waliohudhuria walionyesha shauku kubwa, kana kwamba walioondoka walikuwa wachache mno licha ya changamoto za mtandao na masumubuko mengine ambayo huwa yanatokea kwenye mikutano pepe.

Vipengele Vikuu

Mafunzo yalizinduliwa na hotuba fupi kutoka kwa Anna Kulaya (Mratibu wa Kitaifa wa MKUKI) aliyegusia kuwa janga la UVIKO-19 limekoleza changamoto zinazowapata watu wenye ulemavu. Hatua za udhibiti, hasa kuvaa barakoa na kujiweka mbali na wengine, kumefanya ujumuishi kuwa mgumu zaidi. Baada ya hapo, Dr. Timo Voipio (Mkuu wa Ushirikiano – Ubalozi wa Ufini) alitoa shukrani za awali kwa ujuzi wote na mafunzo yote yaliyotarajiwa kutolewa kwenye warsha.

Yafuatayo yalikuwa malengo ya warsha kama alivyoainisha Patricia Mwaikenda (ELCT):

- Kuelewa misingi ya ufikikaji
- Kuimarisha ufikikaji na upatikanaji wa mawasiliano, matukio, na mikutano ya kampeni ya Siku 16 ya mwaka 2021
- Kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu UWAKI pia zinajumuisha masuala ya ulemavu
- Kubadili/kuboresha miundo ya kampeni zijazo na huduma za huko mbeleni

Baada ya hapo washiriki walisikiliza simulizi fupi ya kutungwa kuhusu Rehema, mwanamke mwenye vilema kadhaa. Mumewe humsaidia na mahitaji ya kila siku lakini pia humnyanyasa. Hii simulizi ilionyesha vikwazo vinavyomzuia Rehema kufikia huduma, na iliwahamasisha washiriki wafikirie ni jinsi gani hali ingekuwa tofauti iwapo Rehema asingekuwa na vilema na asingekuwa mwanamke. Madhumuni ya hii simulizi isiyo halisi ilikuwa kuonyesha muingiliano wa haki za wanawake, haki za walemavu, na UWAKI. Hatimaye, sehemu ya mwanzo ya semina ilimaliziwa na mifano mbalimbali ya UWAKI pamoja na hali zinazowahatarisha zaidi watu wenye vilema ikiwemo:

- Uwezo wa kudhibitiwa kwa jinsia, umri, na aina ya ulemavu
- Ukosefu wa elimu ya ujinsia na uzazi
- Kutoelewa uzito wa uhalifu wa namna hii
- Wanyanyasaji wanaona ngono kama ‘kumwoneysha mapenzi’ mwenye ulemavu
- Imani kwamba ngono na watu wenye ulemavu ni salama au inamfaa mhusika
- Kuongezeka kwa mazingira magumu kupitia utunzaji duni na kutelekezwa

Ufikikaji ni nini?

Ulemavu unaelezeka kama uhusiano baina ya mapungufu ya mtu na mazingira yake. Ufikikaji unapowezeshwa, mapungufu peke yake hayachangii mtu kuwa mlemavu.

Mchoro umetoka CBM International (2017) Accountability Inclusive Development Toolkit
Tafsiri imefanywa na Sylvia K. Ilahuka

Kama ilivyoelezwa na Rafiki Msafiri (Abilis Foundation), ufikikaji ni pale ambapo watu wenye ulemavu huweza kufanya au kupata wanayochohitaji kwa kutumia muda na jitihada sawa na wale wasio na ulemavu. Ufikikaji hudhibitiwa na mikataba, sheria na kanuni za kimataifa na nchi husika, kama vile Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa Umoja wa Mataifa (CRPD). Ufikikaji ni hitaji la baadhi lakini huwanufaisha wote.

Ufikikaji huwezesha ujumuishi.

Makundi tofauti ya ulemavu yana mahitaji tofauti, kwa mfano ngazi mtelezo kwa wenye ulemavu wa viungo, alama za mguso kwa wenye changamoto za uoni, na wakalimani wa lugha ya alama kwa wenye changamoto za usikivu.



Mnyororo wa mzunguko wa ufikikaji

Lengo kuu la ufikikaji, kama alivyoeleza Benjamin Kihwele (Sense International), ni ili kila mtu (wakiwemo watu wenye ulemavu) aweze kuyafikia na kuyatumia mazingira yanayomzunguka kwa kadiri anavyohitaji pasipo kikwazo. Namna za kuboresha na kuhakikisha ufikikaji ni:

- Kutambua tatizo la kila mtu kulingana na ulemavu wake na mahitaji
- Weka mipango ya kufanya maboresho ya ufikikaji kulingana na hitaji lililobainika
- Tekeleza mpango kulingana na mahitaji (Mfano,ujenzi wa miundombinu rafiki,matumizi sahihi ya lugha za mawasiliano, n.k.)
- Tathmini utumiaji na kuendelea kuboresha kulingana na mahitaji.

Katiba imebainisha wazi haki ya kupata habari kwa wote katika ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977. Pia Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2010 kifungu cha 3,38,43 (1) 55,(1) inaelekeza umuhimu na ulazima wa matumizi ya ukalimani ili kuwawezesha viziwi kupata huduma na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii na kimaendeleo. Licha ya haya, bado kuna mapungufu yanayohitaji wadau watie msisitizo yaboreshwe.

Hata yule wa mwisho kabisa akifikiwa, basi watu wote wanakuwa wamefikiwa.

Baada ya hapo, James O'Sullivan (Abilis Foundation) aliwaelekeza washiriki namna za kuwezesha ufikikaji wa maudhui pepe. Walifundishwa namna ya kusanifu kwa ajili ya walio na changamoto za kuona au kusikia, pamoja na namna ya kukidhi mahitaji haya pasipo teknolojia za kisasa au intaneti thabiti. Pia alizingatia kwa kina ufikikaji katika enzi za mitandao ya kijamii, na alishauri kipaumbele kiwekwe kwenye ufikikaji kuanzia mwanzo kabisa wa kubuni badala ya kujaribu kufanya marekebisho baadaye.

- **Sanifu kuendana na changamoto:** uoni, usikivu, mazingira yasio na mtandao au teknolojia ya kisasa
- **Maandiko:** herufi kubwa, rangi zinazoonekana kirahisi, hifadhi katika muundo unaoweza kusomeka kwa kutumia teknolojia saidizi (yaani screen readers)
- **Picha:** weka maelezo ya Alt-Text (yaani maandishi mbadala), tumia picha zinazoonyesha watu wenye ulemavu katika hali nzuri zenye hadhi
- **Kanda:** manukuu, video ya lugha alama pembezoni, kutumia kinasasauti ili kupata usikivu msafi
- **Mitandao ya kijamii:** fuata Mwongozo wa Ufikikaji wa Maudhui Pepe (yaani Web Content Accessibility Guidelines), pia pata maoni ya watumiaji wenyewe.

Nyakati hizi za janga la UVIKO-19, makusanyiko mengi yamehamia mtandaoni – badiliko linalozidisha changamoto za ujumuishi na ufikikaji hasa kwa wale wenye mahitaji ya uoni au kusikia. Tuomas Tuure (Abilis Foundation) aliyetoa maelekezo kuhusu njia bora zaidi za kuhakikisha ufikikaji wa kidijitali kwenye mikutano na matukio pepe, kuanzia kwenye kufanya mipango na kuandaa nyenzo.

- Wezesha uwasilishwaji wa maombi ya awali ya maboresho yo ufikikaji, pia wahushishe wenye ulemavu katika maandalizi ili kuhakikisha ufikikaji mzuri
- Fikiria mapungufu ya mtandao wa intaneti na teknolojia kwa ujumla, hasa kwenye nchi za kusini mwa dunia
- Tumia mialiko jumuishi: usajili rahisi na maelezo marahisi kuhusu tukio na namna ya kujiunga
- Wezesha namna za kushiriki zisizotegemea intaneti ama kompyuta, kwa mfano uwezo wa kushiriki kwa simu
- Kuwezesha usikivu: tumia kinasasauti, vipaza sauti vya masikioni ikiwezekana, na wakalimani wa lugha ya alama
- Kuwezesha uoni: mwanga mzuri, rangi zinazoonekana kirahisi, lugha ya mguso, mabango makubwa
- Andaa nyenzo zote katika muundo unaofikika na zigawe kwa washiriki kabla ya shughuli
- Karibisha maoni na mapendekezo ya maboresho, kwa kuwa ufikikaji ni somo linaloendelea daima

Kufuatia masomo hayo, washirikia waligawanywa katika makundi manne (4) ili kutafakari maswali yafuatayo na kuyajibu:

Swali	Jibu
Kikundi 1: Unahusika na kuandaa mpango wa media wa kitaifa wa Kanda ya Ziwa kwa Siku 16 za Uanaharakati kumaliza Ukatili dhidi ya Wanawake 2021. 1. Je! Unamshirikisha nani katika maandalizi? 2. Je! Mpango wako wa mawasiliano kwa ujumla unaonekanaje kuhakikisha upatikanaji? 3. Bajeti inapaswa kuzingatia nini ili kuwa jumuishi?	1. Wadau, na hasa wenye ulemavu wenyewe ili kutambua mapungufu yaliyopo 2. Chagua njia ya mawasiliano inayoendana na mahitaji au changamoto za walengwa 3. Bajeti izingatie miundombinu yenye kufikika, pamoja na uwakilishi tosha wa kijinsia.
Kikundi 2: Unahusika na kupanga hafla ya uzinduzi wa kitaifa wa Siku 16 za Uanaharakati. 1. Unaiandaa wapi? 2. Unawaalika akina nani? 3. Ulikuwa na maoni gani ya bajeti kuhakikisha upatikanaji?	1. Mahala patakapofikika na kutumika kirahisi na wahudhuriaji wenye ulemavu 2. Wenye majukumu, mf. serikali, viongozi wa kidini, wanasiasa, wanahabari, watoa huduma kwa wenye ulemavu, mashirika ya walemavu, mashirika ya vikundi vingine kama wanawake/watoto 3. Bajeti izingiatie upatikanaji halisia na pepe (mfano vipeperushi, vibao vya maelekezo, wakalimani wa TAL, n.k.)
Kikundi 3: Unahusika na kuandaa hafla ya Msafara wa Mabadiliko kwa Siku 16 za Uanaharakati. Hii ni basi iliyojaa wanaharakati ambao hupitia Tanzania nzima ili kuongeza uelewa na kusikiliza sauti za jamii kwenye UWAKI. 1. Je! Unamwalika nani kwenye vituo vya mkoa? 2. Bajeti yako inaonekanaje?	1. Viongozi was mkoa na serikali za mitaa, maafisa jamii wa ngazi mbalimbali, wazee wa kimila, waganga wa jadi, vyama vya akina mama, vikundi vya bodaboda, wazazi (hasa wazazi wa watoto wenye ulemavu), wadau wa mitandao ya kijamii, wafungwa 2. Bajeti inagharimia wakalimiani wa TAL, matangazo kwenye vyombo vya habari na pia kwenye mitandao ya kijamii

Kikundi 4: Unashiriki katika kuunda ujumbe wa media karibu na uHii ni basi iliyojaa wanaharakati ambao hupitia Tanzania ili kuongeza uelewa na kusikiliza sauti za jamii kwenye UWAKI. Unashiriki katika kuunda ujumbe wa media karibu na ulemavu na GBV kwa siku 16 za Uanaharakati. 1. Fikiria ujumbe 2-3 unaoweza kuwagusa wanasera wa UWAKI 2. Fikiria ujumbe 2-3 kuigusa jamii kwa ujumla 3. Fikiria ujumbe 2-3 ambao unaweza kuwafahamisha watu wenye ulemavu kuhusu haki yao ya kuishi bila vurugu	1. Watu wenye ulemavu wana haki saw ana wengine, washirikishe katika maeneo yote ya kuunda sera, mf. bungeni, serkali za mitaa, kwenye jukwaa za jamii na za kitaifa Haki za walemavu ni haki za binadamu, msitubague! 2. Wanawake wenye ulemavu wasiachwe nyuma, wajumuishwa na kushirikishwa Kuwa na mtoto mwenye ulemavu si laana wala aibu, usiwafungie ndani, wahusishe katika maeneo yote ya maisha ya kawaida Achana na imani potofu kuhusu watu wenye ulemavu, mf. albino 3. Hakuna chetu bila sisi! Daini haki zenu! Chukua hatua kuwanusuru walemavu kwenye UWAKI.

Kazi ya vikundi ilipomalizika, James O'Sullivan (Abilis Foundation) aliwelekeza washiriki kwenye tovuti za ziada wangezoweza kurejea ili kuendelea kujifunza kuhusu upatikanaji na ujumuishi.

Nyenzo kutoka Fingo
https://fingo.fi/en/fingo-powerbank/learning-material/technology-and-digital-accessibility-toolkit-for-ngos/

Nyenzo za Ufikikaji wa Kidijitali kutoka CBM
https://www.cbm.org/fileadmin/user_upload/Publications/CBM-Digital-Accessibility-Toolkit.pdf

Mawasiliano Jumuishi, Mwongozo kutoka Umoja wa Mataifa
https://www.unicef.org/peru/sites/unicef.org.peru/files/2021-10/un_disability-inclusive_communication_guidelines.pdf

Miundo ya Mwasiliano Fikika kutoka Serikali ya Uingereza
https://www.gov.uk/government/publications/inclusive-communication/accessible-communication-formats

Ya Kufanya na ya Kuepuka wakati wa Kusanifu kwa ajili ya Ufikikaji
https://accessibility.blog.gov.uk/2016/09/02/dos-and-donts-on-designing-for-accessibility/

Ufikikaji GO! Mwongozo wa Matekelezo
https://worldblindunion.org/wp-content/uploads/2021/04/Accessibility-GO-A-Guide-to-Action-WBU-CBM-Global.pdf

(Picha zimetolewa na Abilis na TCRS)

Kwa kuwa muda uliosalia haukua mwingi, kipindi cha maswali na majibu kilifutwa; badala yake lilitolewa neno la shukrani na Aginatha Rutazaa (Tusonge Community Development Organisation).
Warsha ilifungwa rasmi na Aneth Gerana (Mkurugenzi - FUWAVITA) na Maja Hansen (UNFPA). Gerana, aliyeungwa mkono na mkalimani wa TAL, alisifu ujumuishi wa semina – hasa kwa kuwepo kwa wakalimani. Alizungumzia huzuni juu ya kifo cha mwanaharakati wa ulemavu Blandina Sembu, akidhihirisha umuhimu wa kukazana na juhudi dhidi ya UWAKI na kuwasihi wadau waendelee kutetea haki za walemavu. Pia alisisitiza namna huduma nyingi za kijamii, kama polisi na huduma za UVIKO-19, hutumia mawasiliano ya maongezi ya simu wakitangaza “piga namba hii” huku Viziwi wengi hawawezi kutumia vema muundo huo wa mawasiliano. Alimaliza kwa kuhimiza ufikikaji na ujumuishi kwenye kampeni ya Siku 16 ya mwaka 2021. Hansen alifuatia kwa kutoa shukrani kwa niaba ya UNFPA na kusisitiza malengo na miradi ya shirika kwenye juhudi za kuukomesha UWAKI.

Muhtasari

- Hakuna kinachotuhusu bila kutuhusisha: ili kuhakikisha ufikikaji kamilifu, wahusishe watu wenye ulemavu katika kupanga na kuandaa matuko na maudhui.
- Ufikikaji huwezesha ujumuishi

- Hatua za kujikinga na janga la UVIKO-19 (kama vile uvaaji wa barakoa, kujiweka mbali na wengine, na kupata huduma kwa simu) kumezidisha vizuizi vya ufikikaji na ujumuishi.
- Madhara ya kijamii na kiuchumi yamechangia mwongezeko wa matukio ya UWAKI, na wale wenye ulemavu huendelea kuwa katika hatari kubwa zaidi.
- Mawasiliano pepe na mikusanyiko pepe huhitaji maboresho ya ufikikaji na upatikanaji.

Ufikikaji wa maeneo/majengo = kuweza kupafikia, kuingia, kuzunguka, na kutumia; ngazi mtelezo, mabango ya maelekezo, mwanga mzuri, njia pana, nafasi ya kutosha viti vya magurudumu

Ufikikaji wa mawasiliano = herufi kubwa, rangi zinazoonekana, maelezo ya Alt-Text, picha zinazowaonyesha watu walemavu katika hadhi nzuri, video ya wakalimani wa lugha ya alama pembezoni

Ufikikaji wa kidijitali = usajili rahisi, sauti safi, mwanga mzuri, namna za kushiriki zisizohitaji mtandao wa intaneti, malezo ya video katka maandishi

(Picha zimetolewa na Abilis, Fida, na TCRS)

Kusonga Mbele

- **Hakikisha utekelezaji wa nyenzo za ufikikaji katika Siku 16 za Uanaharakati 2021.** Ujuzi uliopokelewa kwenye mafunzo haya lazima yatumike kwenye kampeni nzima, yaani masomo yageuzwe kuwa vitendo.
- **Mafunzo ya mbeleni yapatikane katika lugha mbalibali.** Warsha hii ilifanyika katika lugha tatu: Kiingerza, Kiswahili, na Lugha ya Alama Tanzania (LAT), huku washiriki wakitafsiriana pale ambapo kuna ambao hawakuelewa. Katika kutafsiriana bila mpangilio rasmi, kuna athari ya kutotafsiri kikamilifu au kukosea kwa bahati mbaya. Hivyo imependekezwa kuwa katika semina zijazo, masomo yapatikane katika Kiingereza na Kiswahili ili kuwawezesha washiriki wote kufuatilia kirahisi na kwa usahihi.
- **Hakikisha uimarishaji kwa kufanya mafunzo endelevu ya kina, na utathmini.** MKUKI wangependa mafunzo ya ziada huko mbeleni. Ikiwezekana, masomo yawe machache ili kuwezesha maelekezo ya kina zaidi. Pia ilipendekezwa kuwa tathmini ifanyike baada ya Kampeni ya Siku 16 2021 ili kupima ni nyezo zipi zilitumika na kwa kiwango gani.

- **Wapatie washiriki vifaa vya kujisomea na ripoti za mafunzo ili kusambaza ujuzi.** Aginatha Rutazaa (Tusonge Community Development Organisation) aliomba nyenzo za mafunzo zipatikane baada ya mafunzo kama haya, ili washiriki waweze kuyarejea kwa muda wao. Aliwasihi waendelee kutafakari juu ya mapungufu katika ufikikaji ili waendelee kujiboresha. Pia ilipenedekezwa kuwa fursa kama hizi zitangazwe kwenye mitandao ya kijamii ili kuongeza uelewa, ushiriki, na mafunzo mengine kama haya.
- **Tengeneza fursa za kuendelea kujifunza.** Rutazaa pia alipendekeza uwezekano wa kipindi cha masomo endelevu ya ushirikiano ili kuimarisha elimu iliyopatikana.

Shukrani

Mafunzo ya yalitolewa na MKUKI na WiLDAF kwa msaada wa Abilis Foundation, ELCT, Felm, Fida International, Sense International, na UNFPA. Ripoti hii inapatikana katika Kiswahili na Kiingereza, na imeandaliwa na Sylvia K. Ilahuka.

Washirika

Abilis Foundation hudhamini miradi inayokuza Haki za Binadamu, ushirikiano, kuishi kwa kujitegemea, elimu, na kuajiriwa kwa Watu wenye Ulemavu katika nchi zinazoendelea, Msisitizo maalum huwekwa kwa washichana na wanawake.

ACT Alliance ni muungano mkubwa zaidi wa makanisa ya Kiprotestanti na Orthodox pamoja na mashirika ya kikanisa yanayojihusisha na kazi haki, maendelo, na uanaharakati ulimwenguni. Muungano una wanchama zaidi ya 130, wakifanya kazi katika nchi zaidi ya 120 kuleta mabadiliko katika maisha ya masikini na waliobaguliwa. Shirikisho la ACT Tanzania kina wanachama 12, wakiwemo wanachama 3 wenyeji, 6 wa kimataifa, na wasimamizi 2.

Kanisa la Kiinjili la Kiluteri Tanzania (KKKT) ni shirikisho la makanisa ya Kiluteri Tanzania linalowapa watu fursa za kuabudu, kupata elimu ya Kikristu, na huduma za jamii kama afya, elimu ya UKIMWI, na msaada baada ya majanga.

Felm ni shirika la Kanisa la Kiinjili la Kiluteri Finland (ELF) linalofanya kazi za kimataifa. Felm hufanya kazi katika nchi 30 kwa sasa, ikishirikiana na makanisa na mashirika zaidi ya 100. Kama moja ya mashirika makubwa ya Kifini yanayofanya kazi za maendeleo dunia, Felm hufadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufini.

Fida International ni shirika la Kifini la kiimani lifanyalo kazi katika maendeleo ya kijamii na msaada wa kibindamu katika nchi 50. Tunalenga kuleta matumaini na kuboresha maisha yajayo kwa nchi zote – hasa kwa watoto waishio katika umaskini.

MKUKI ni mtandao unaojumuisha mashirika 70 ya Kitanzania, yanayochangiana katika kudumisha lengo la kukomesha ukatili wa kijinisia katika maeneo ya vijijini na mijini.

Sense International ni shirika linalotoa misaada kwa watu wenye uziwipofu katika nchi za Bangladesh, India, Kenya, Nepal, Tanzania, Peru, Romania, na Uganda.

UNFPA ni shirika la afya ya uzazi la Umoja wa Mataifa. Dhamira yetu ni kufikia ulimwengu ambapo kila ujauzito ni wa kutakwa, kila kujifungua ni salama, na uwezo wa kila kijana unatimizwa.

Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) ni mtandao wa Kiafrika wa haki za wanawake unaojitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo, ili kuongeza ushiriki na ushawishi wa wanawake katika ngazi za kijamii, kitaifa, na kimataifa.

Waliohudhuria

- Abilis Foundation
- ACT Forum Tanzania
- Civic and Legal Aid Organisation
- Comprehensive Support to Persons with Disabilities (COSUPED)
- Door of Hope Tanzania
- Embassy of Finland - Tanzania
- Engender Health
- Evangelical Lutheran Church in Tanzania (ELCT)
- Felm
- Fida International
- Finnish Mission - Kenya
- Finnish Mission - Uganda
- Free Pentecostal Churches of Tanzania (FPCT)
- Full Gospel Church Kenya
- Furaha Ya Wanawake Wajasiriamali Kwa Viziwi Tanzania (FUWAVITA)
- Global Peace Foundation Tanzania
- HIMIZA Development
- Health Integrated Multisectoral Services (HIMS) Arusha
- Kimamba Youth Organisation
- Morogoro Paralegal Centre
- Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Mkoa wa Kilimanjaro (MVIWAKI)
- Mwanasatu Development Organization (MWADO)
- Mwanza Youth and Children Network (MYCN)
- Sauti ya Haki Tanzania
- Save Community Health Initiative (SACOHEI)
- Save the Children
- SDA Special School for Learners with Intellectual Disability Kenya
- Sense International - Tanzania
- Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA)
- Sign Language Interpreters
- Tanganyika Christian Refugee Service (TCRS) - Kilwa Office
- Tanzania Ministry of Health, Community Development, Gender, Women, and Children
- Transformative and Integrative Build Out for All (TIBA)
- Tusonge Community Development Organization - Moshi
- United Nations Population Fund (UNFPA)
- Waking the Giant Initiative
- Women and Children Welfare Support (WOCWELS)
- Women in Law and Development in Africa (WiLDAF)
- Women in Mining Association
- Women Promotion Centre
- Women Wake Up (WOWAP) Dodoma
- Youth with Disabilities Community Programme
- Youth with Disabilities Organisation
- Youth Partnership Countrywide (YPC) - Kibaha

Hakuna kinachotuhusu bila kutuhusisha!